**JAMUHURI YA MUUNGANO TANZANIA**

**OFISI YA RAISI –TAMISEMI**

SHULE YA
SEKONDARI KITOMANGA,
S.L.P 464,
LINDI.
10/12/2020.

Ndg; ……………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI KITOMANGA -2021**

Kwanza natumia fursa hii kukupongeza kwa kufanya vizuri katika mtihani wa darasa la saba mwaka 2020. Pili napenda kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari kitomanga. Shule ya sekondari kitomanga ni shule ya kutwa na ni shule ya mchanganyiko (wasichana na wavulana).
Pamoja na barua hii kuna viambatanisho vifuatavyo lazima uvisome na kuvifanyia kazi;

- **Fomu namba 1- sheria za shule**
- **Fomu namba 2- mahitaji ya mwanafunzi**
- **Fomu namba 3- kukubali au kukataa nafasi uliyopewa**
- **Fomu namba 4 – kupima afya.**

Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 **,** kumbuka kuwa usajili utaanza siku ya kufungua shule yaani tarehe 11/01/2021 hadi 18/01/2021 ili masomo yaanze haraka iwezekanavyo.
Mwisho, nawatakia maandalizi mema na safari njema ya kuja shuleni.

…………………………………………………..
BAHIA T ABUBAKAR
MKUU WA SHULE
KITOMANGA SEKONDARI

**FOMU NO. 1**

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI KITOMANGA.

MOTO WA SHULE. **ELIMU NI UFUNGUO WA MAFANIKIO KATIKA MAISHA.**

Ili kumjenga mwanafunzi katika taaluma, maadili na muelekeo unaobadilika katika jumuiya yake ya leo na baadae kanuni na sheria zifuatazo inabidi zitekelezwe na kila mwanafunzi;

1. Mwanafunzi anapaswa kuwahi na kufuata ratiba inayomuhusu wakati wote awapo shuleni.
2. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare inayokubalika na shule kufuatana na ratiba iliyopo kila wakati
3. Ni mwiko kupiga kelele katika eneo la shule
4. Kazi ni kipimo cha utu- mwanafunzi atafanya kazi alizopewa kwa bidii na maarifa hadi kukamilisha kadri alivyoelekezwa
5. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja yakidhihirika;
    - Uasherati
    - Kupata mimba au kumpa mwanafunzi mwenzake mimba
    - Kumpiga yeyote (kupigana)
    - Ulevi na Kutumia ama kuuza madawa ya kulevya
    - Wizi wa aina yeyote
    - Wizi wa Mitihani au kufanya udanganyifu wakati wa mitihani ya aina yoyote
    - Kumiliki ,kutumia au kukutwa na SIMU
    - Kuhamasisha MGOMO au vurugu ya aina yeyote
6. Heshima ni jambo la muhimu katika jamii,mwanafunzi anatakiwa kusalimia watu wote waliomzidi umri kadri ya stahili zao, pia aonyeshe heshima kwa wanafunzi wenzake na jamii yote.
7. Mwanafunzi harusiwi kuonekana maeneo ya starehe za jamii. Mfano bar, nyumba za kulala wageni (guest house) na disko hata kama yupo nyumbani.
8. Siku za shule zote mwanafunzi awapo shuleni atatoka nje ya shule kwa kibali maalumu, ruhusa itatolewa na makamu mkuu wa shule kwa maombi ya maandishi, wenye ruhusa watatakiwa kuvaa sare za shule katika safari zao.
9. Kwa vile masomo yote hufundishwa kwa kiingereza isipokuwa Kiswahili tu, mawasiliano yote ya kikazi yafanyike kwa kiingereza isipokuwa ukielekezwa vinginevyo.
10. Lugha chafu ni mwiko (matusi) unapaswa kuwa safi kimwili, kimavazi na katika lugha yako.
11. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

OFISI YA RAISI –TAMISEMI
MKOA WA LINDI
SHULE YA SEKONDARI KITOMANGA

FOMU NO.2

A. VIFAA VYA DARASANI.
- Madaftari(counter books) yasiyopungua kumi na mbili (12) au zaidi, mkebe, kalamu za kutosha na file la plastiki.
- Begi la kuwekea daftari.
- Daftari ndogo 10 kwa ajili ya test na mazoezi kwa kila somo.
- Kamusi English – Kiswahili.
- Ream 1 kwa ajili ya mitihani ya kila juma.

B. SARE ZA SHULE

1.WAVULANA
- Suruali mbili ndefu za rangi NYEUSI (isiwe modal)
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi (aina ya tomato)
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili
- Tai nyeusi

2 . WASICHANA
- Sketi mbili rangi ya NYEUSI ( nzito inayovuka magoti)
- Shati nyeupe mbili mikono mifupi kwa wasiovaa hijabu.(aina ya tomato)
- Na kwa wanaovaa hijabu NUSU KANZU
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu
- Soksi nyeupe jozi mbili.

SHAMBA DRESS (MAVAZI YA WAKATI USIOKUWA WA MASOMO).

1.WAVURANA.
- Suruali 1 rangi ya damu yam zee (ISIWE MODAL).
- T- shirt 1 ya blue ambayo ina nembo ya shule.

2.WASICHANA.
- Sketi 1 rangi ya ugoro (nzito inayovuka magoti).
- T- shirt 1 rangi ya blue ambayo ina nembo ya shule.

C. MAHITAJI YA VIFAA VYA MICHEZO NA USAFI. (KWA WANAFUNZI WOTE)
- Bukta ama track suit rangi ya blue.
- Viatu (raba) na soksi jozi mbili za michezo
- Jembe lenye mpini (ngwamba)
- Fyekeo au panga
- Ndoo ndogo moja.
- Fagio la chelewa.

**D: MAHITAJI YA KIAFYA.**
- Aje na bima ya afya.

**SHULE YA SEKONDARI KITOMANGA**

**FOMU NO.3**

**A. YAH: KUKUBALI/KUKATAA NAFASI (MWAFUNZI)**

**Mimi ………………………………………………………………………….. nakiri kopokea barua ya kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari katika shule ya sekondari kitomanga. Baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu hii NIMEKUBALI NAFASI/NIMEKATAA NAFASI ya kuendelea na masomo.**

**Ninahaidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule. Kamwe sitoshiriki au kujihusisha na vitendo vya uvunjaji wa sheria za shule na makosa mengine ya jinai.**

**Nitatumia juhudi na maarifa katika kujifunza kwa manufaa yangu, wazazi, jamii na taifa kwa ujumla. Aidha ninahaidi kuwepo shuleni muda wote na endapo itatokea nataka kutoka nje ya shule nitaomba ruhusa na kuvaa sare rasmi za shule.**

**Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………………saini ……………..tarehe……………………**

**Jina la mzazi/mlezi ……………………………………………..saini……………………..tarehe…………**

**B. MAKUBALIANO YA MZAZI/MLEZI.**

**Mimi ……………………………………………. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……………………..……………………**

**Wa kidato cha ……………… mwaka …………………….. ninakubaliana na masharti tajwa hapo juu, hivyo naahidi kutekeleza mkataba huu na kuamuru mwanangu autekeleze. Endapo mwanangu atashindwa kutekeleza basi sheria ifuate mkondo wake.**

**NB: Wasiliana na uongozi wa shule kwa ufafanuzi zaidi kwa namba 0786763078- MKUU WA SHULE au 0784776554 (MAKAMU MKUU WA SHULE)**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

**……………………………………………………..**

**BAHIA T ABUBAKAR**

**MKUU WA SHULE**

**KITOMANGA SEKONDARI**

**Fomu na 4.**

**PRESIDENT'S OFFICE,**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**KITOMANGA SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.BOX 464,**
**Lindi.**

REF: NO ………………………………..
To The Medical Officers (District/regional)
…………………………………………………………..
Sir/Madam,

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO**
(***Name of student)…………………………………………………………***

Please examine the above named student and give the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school studies.

1. Student's full name……………………………………………………………………………………
2. Blood…………………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………………………………
3. Stool…………………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………………………………..
4. T.B test ……………………………………………………………………………………………………
5. Syphilis test…………………………………………………………………………………………….
6. Urine examination……………………………………………………………………………………..
7. Eyes test ……………………………………………………………………………………………………..
8. Chest test……………………………………………………………………………………………….
9. Earstest…………………………………………………………………………………………………
10. Spleen…………………………………………………………………………………………………… ……………………………………………………………………………………………………..
11. Abdomen……………………………………………………………………………………………….
12. Pregnancy (for girls only)……………………………………………………………………………

**ANY ADDITIONAL INFORMATION : EG Physical defects or impairment, infection, family diseases** etc
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………………

COMMENTS:…………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………….

I certify that the above student is suitable/unsuitable for secondary school studies. If unsuitable give reasons
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
…………………………

**Name of Medical Officer**……………………………………………………**Signature** ………………………

**Date**……………………………………………………………….. **Official stamp** ………………………………